Candidate's Number _____

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION

FORM TWO SECONDARY EDUCATION EXAMINATION,1989

0011 ELIMU YA SIASA

MUDA: SAA 2.

Jibu maswali YOTE katika karatasi hii.

Andika Namba yako ya mtihani katika kila ukurasa.

1. Katika swali hili lenye vipengele (i) - (xx) kuna majibu manne kwa kila kipengele. Chagua jibu sahihi zaidi kwa kila kipengele na kuandika herufi yake katika nafasi iliyoko kando ya kila kipengele.

Mfano:

Mfumo wa awali wa maisha ya jamii ulikuwa:

A. Ubepari
B. Ujima
C. Ujamaa (B)
D. Ukabaila

(i) Zipi kati ya sentensi zifuatazo zinaeleza kwamba kuu tatu za maisha ya ujima:

A. Kupendana, kuheshimiana, kushi pamoja.
B. Kumiliki mali pamoja, kupendana, kila mtu kufanya kazi ( )
C. Kupendana, kumiliki njia kuu za uchumi,
D. Kupendana, kufanya kazi pamoja, kuishi kijamaa.

(ii) Utaratibu wa mwanzo kabisa wa maendeleo ya binadamu ulikuwa duni kwa sababu:

A. Uwezo wa kivango cha kuzalisha mali ghafi ulikuwa mdogo.
B. Wamawake hawakufanya kazi za kuzalisha mali isipokuwa kazi za nyumbani
C. Sayansi na Teknolojia yao ilikuwa duni. ( )
D. Ngazi za kiuongozi hazikujulikana.

(iii) Jamii za kiafrika zilikuwa zimepiga hatua mbalimbali za kimaendeleo, kabla ya kuja kwa wageni. Moja ya hatua hizo ni kuwa na utaratibu wa kudumu wa kiuongozi, ambao hapa kwetu Tanzania ulijitokeza Qazi katika jamii zifuatazo:

A. Wanyamwezi, Wahehe na Wachagga
B. Wasambaa, Wabarabaig, Wahehe
C. Wangoni, Wasandwawi, Wamasai ( )
D. Wanyamwezi, Wanyiramba, Watindiga

(iv) Wavamizi wa kwanza wa kikoloni nchini Tanzania ni :

A. Waremo
B. Waingereza
C. Wajerumani ( )
D. Waarabu

Candidate's Number_____

(v) Waingereza walisifika kwa kuwa na mazudo wa utawala uliojulikana kama:

A. Utawala wa moja kwa moja.

B. Utawala wa kifalme.

C. Utawala wa mlango wa nyuma

D. Utawala wa moeto. ( )

(vi) Matokeo ya vita vikuu vya kwanza vya dunia kwa Watanganyika yalikuwa:

A. Jumuiya ya mataifa ilikabidhi nchi kwa waingereza

B. Wajerumani walipewa masharti na jumuiya ya Mataifa juu ya kuiongoza Tanganyika.

C. Jumuiya ya mataifa ilituma ujumbe rasmi nchini kuorodhesha dosari zote za utawala uliokuwepo. ( )

D. Wananchi walipata mwamko katika kutafuta mbinu mpya za kupigana na ukoloni mkongwe.

(vii) Chama cha Tanu kilianzishwa kwa madhumuni ya:

A. Kupinga serikali ya moeto nchini

B. Kuwatayarisha wananchi wajitawale

C. Kuelezea kisiasa madhumuni ya chama cha T.A.A ( )

D. Kuondoa dosari za kibaguzi zilizokuwepo katika vyama vingi vya kisiasa nchini.

(viii) Kuenea haraka kwa chama cha TANU nchini kulitokana na:

A. Kutokuwepo kwa vyama vilivyoipinga TANU

B. Wazungu walikuwa wachache sana

C. Siasa yake thabiti na uongozi bora wa Mwalimu J.K Nyerere ( )

D. Lugha ya kiswahili ambayo ilitumika kwa Tanganyika pamoja na uongozi bora wa chama chini ya Mwalimu.

(ix) Vyama vya upinzani kwa S.A.S.P vilikuwa:

A. Z.N.P na Z.P.P.P

B. D.P na Z.P.P.P

C. Umma Party na D.P ( )

D. U.T.P na Z.N.P

(x) Moja ya chabaha za Azimio la Arusha ni:

A. Kuleta usawa wa kiuchumi nchini

B. Kuondoa viongozi wabadhirifu katika chama

C. Kuweka misingi ya kumiliki njia kuu za uz-lishajimali ( )

D. Kutekeleza siasa ya ujamaa na kujitegemea kwa vitendo.

(xi) Moja kati ya matatizo katika Azimio la Arusha ni.

A. Kukosa fedha za kigeni

B. Kushindwa kuelewa na kutekelza mambo yote yenye kujenga tabia ya kujitegemea.

C. Kutokuwepo miongozo iliyo wazi ya kufuatwa baina ya wananchi na viongozi. ( )

D. Kuendelea kuwepo kwa shughuli za uzalishaji mali za watu binafsi.

(xii) Azimio la Arusha limegawanywa katika mehemu kuu:

A. Tatu

Candidate's Number _____

B. MBILI
C. Sita
D. TANO ( )

(xiii) Sababu kubwa ya kuundwa kwa chama cha Mapinduzi nchini Tanzania ni
A. Kuimarisha mshikamano wetu
B. Kulinda uhuru na heshima ya watu wa visiwani na Tanzania bara.
C. Kuwa na msimamo mpya wa kimapinduzi hasa katika muundo wa kiongozi. ( )
D. Kuwa na chama kimoja chenye lengo moja la kijamaa.

(xiv) Uhai wa chama unatokana na:
A. Michango ya hiyari ya wanachama.
B. Kulipia ada ya chama bila kuchelewa kila mwezi
C. Kuwepo kwa vikao vya chama kwa mujibu wa katiba ( )
D. Kuielewa vizuri katiba ya chama.

(xv) Ikitokea kwamba kiti cha Rais kiwazi kutokana na sababu yoyote au Rais hayupo katika Jamhuri ya Muungano kikazi, kazi zake zinaweza kushikwa na mmoja kati ya watu wafuatao:
A. Makamu 1 wa Rais, Waziri Mkuu, Jaji Mkuu, Spika wa Bunge.
B. Makamu 1 wa Rais, Makamu wa 11 wa Rais, Waziri wa mambo ya Nchi za Nje.
C. Spika wa Bunge, Jaji kiongozi, Waziri Mkuu, Makamu 1 wa Rais. ( )
D. Makamu wa 1 wa Rais, Makamu wa 11 wa Rais, Spika wa Bunge, Jaji Mkuu.

(xvi) Bunge la Jamhuri ya Muungano limegawanyika katika sehemu kuu:
A. Sita
B. Mbili
C. Tatu ( )
D. Nne

(xvii) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hufanya mambo makuu matatu ambayo ni:
A. Kutunga sheria, Kuhukumu wahalifu, kuelimisha umma.
B. Kulinda usalama wa Rais, kutunga sheria, kuweka mikataba na nchi za nje ili kupata fedha za kigeni. ( )
C. Kutunga sheria, kuhukumu wahalifu, kulinda usalama wa raia.
D. Kulinda usalama wa raia, kutoa huduma muhimu, kuhumu wahalifu.

(xviii) Wazo lolote linalokusudiwa kuwa sheria, kabla halijawasheria huitwa muswada. Kuna aina tatu za muswada, ambazo ni:
A. Muswada wa Serikali, wa mjumbe, wa binafsi.
B. Muswada wa serikali, wa wabunge, wa baraza la wawakilishi
C. Muswada wa binafsi, wa mjumbe, wa mashirika ya umma. ( )
D. Muswada wa serikali, wa binafsi, maalum.

Candidate's Number _____

(xix) Watanzania tupo katika vugavuga la kutekeleza kanuni ya maingi katika utendaji kazi, iitwayo "uwajibikaji". Wazo hili limepata mkazo mkubwa kutokana na.

A. Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na la mwaka 1986.

B. Agizo la mwenyekiti wa chama la 1986

C. Agizo la halmashauri kuu ya Taifa la 1986. ( )

D. Agizo la Mkutano Mkuu wa chama wa pili wa kawaida wa mwaka 1982.

(xx) Madaraka mikoani ni utaratibu wa utawala uliowakabidhi wananchi uwezo wa kujiamulia mambo yao wenyewe. Utekelezaji wa utaratibu huo umekumbwa na matatizo mengi ya kiutekelezaji. Moja ya matatizo hayo ni:

A. Kukosekana kwa fedha za kigeni za kuendeshea mipango

B. Muundo wa mgawanyo wa kazi na madaraka kwa viongozi ulichelewesha utekelezaji wa mipango iliyowekwa. ( )

C. Mawazo ya viongozi katika ngazi za vijiji hayakutiwa maanani

D. Kutegemea mno fedha toka se ikali kuu ili kuendeshea mipango.

2. Katika sentenso zifuatazo andika K baada ya sentenso ambayo ni kweli na S baada ya ile ambayo ni kweli.

(a) Ukoloni mkongwe ni kutawaliwa na Taifa jingine kiuchumi na kijeshi 6

(b) Tarehe 5/2/1987 tuliadhimisha sikukuu ya kuzaliwa kwa Azimio la Arusha na CCM.

(c) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar ndiye Rais wa Zanziba _____

(d) Mkutano Mkuu wa Taifa ndicho kikao kikuu cha chama kupita vyote nandicho chenye madaraka ya mwisho _____

(e) Tume ya uchaguzi humpendekeza mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano _____

(f) Azimio la Musoma linasisitiza kilimo na ufugaji bora hapa nchini _____

(g) Mwingereza alitutawala kabla ya Mjerumani _____

(h) Ukabaila ni mfumo wa kwanza wa unyonyaji katika maendeleo ya binadamu _____

(i) Wabunge wa kuteuliwa na Rais ni wale wanaoshindwa kupata kura za wananchi _____

(j) Anayetaka kujiunga na CCM lazima awe raia wa Tanzania _____

Candidate's Number _____

3. Oanisha vifungu vya maneno vya kundi "A" na vile vya kundi "B" ili vilete maana inayokusudiwa kwa kuandika namba 20 kundi "B" kwenye nafasi wazi kando ya kundi "A".

KUNDI "A"

(a) Mtindo ambao watu wachache humiliki ardhi ( )
(b) Kupeleka madaraka kwa wananchi ( )
(c) Kuto fungamana na upande wowote ( )
(d) Ubepari uliokomaa ( )
(e) Mkutano Mkuu wa Taifa ( )
(f) Kamati kuu ya Halmashauri kuu ya Taifa ( )
(g) Demokrasi ( )
(h) Kamati ya Mkutano Mkuu wa Taifa ( )

KUNDI " B"

(a) 1. Ubepari

2. Kubadili katiba ya chama
3. Utawala wa watu wenyewe
4. Elimu ya kujitegemea
5. Bunge
6. Ukabaila
7. Ubepari
8. Siasa ya ujamaa ya Tanzania
9. Serikali za mitaa.
10. Utekelezaji wa shughuli za kila siku za chama.

4. (a) Taja shabaha tatu za Mapinduzi ya zanzibar January 12, 1964
(i) _____
(ii) _____
(iii) _____

(b) Katika kujitafutia makoloni, mabepari walikuwa na madhumuni yafuatayo:-
(i) _____
(ii) _____
(iii) _____

(c) Wajibu wa Chama cha kijamaa ni kuongoza shughuli zote za Umma. Kuongoza maana yake ni:-
(i) _____
(ii) _____
(iii) _____

5. Kamilisha habari ifuatayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi a - j.
Aina za wanachama wa CCM ni (a) _____ na (b) _____. Mtu anayetaka kuwa mwanachama ajiunge (c) _____ na kupeleka kwa (d) _____ Chama, hupewa (e) _____ ya kutosha juu ya (f) _____ , (g) _____, na nia na ya Chama kwa jumla. Mtu akifaha kubaliwa kuwa mwanachama, inambidi kutoa (h) _____, (i) _____ kufuata masharti ya chama na kutekeleza (j) _____ ya Chama.

Candidate's Number_____

6. Eleza kwa kifupi maana ya dhana zifuatazo:

(a) Kujitegemea ____

(b) Ujima ____

(c) Ukupe ____

(d) Katiba ____